JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# MWONGOZO WA UTAHINI NA UTUNUKU KWA KUZINGATIA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 TOLEO LA MWAKA 2023 NA MITAALA ILIYOBORESHWA

**Umeandaliwa na;**
**Baraza la Mitihani la Tanzania**
**S. L. P. 2624**
**Dar es Salaam**

**Agosti, 2024**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# MWONGOZO WA UTAHINI NA UTUNUKU KWA KUZINGATIA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 TOLEO LA MWAKA 2023 NA MITAALA ILIYOBORESHWA

Umeandaliwa na;
Baraza la Mitihani la Tanzania
S. L. P. 2624
Dar es Salaam

**Agosti, 2024**

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ..... iv

1.0 UTANGULIZI ..... 1

2.0 UPIMAJI NA UTAHINI UTAKAOFANYWA NA BARAZA LA MITIHANI ..... 3

3.0 KUTUNUKU UPIMAJI WA KITAIFA NA MITIHANI YA TAIFA ..... 23

3.1 Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Pili (STNA) ..... 23

3.2 Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) na Darasa la Sita (SSNA) ..... 23

3.3 Upimaji wa Kitaifa Kidato cha Pili (FTNA) na Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) ..... 24

3.4 Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita (ACSEE) ..... 30

3.5 Mitihani ya Stashahada za Ualimu ..... 32

4.0 UTARATIBU WA KUTUNUKU VYETI ..... 36

5.0 UTHIBITI NA USIMAMIZI WA ALAMA ENDELEVU ..... 36

5.1 Usimamizi wa Upimaji na Mitihani Ngazi ya Shule ..... 36

5.2 Ujazaji na Uwasilishaji wa CA za Wanafunzi/ Wanachuo ..... 37

5.3 Upimaji na Upatikanaji wa Alama za Kazi Mradi ..... 38

5.4 Ufuatiliaji na Tathmini ya Alama Endelevu ..... 39

6.0 HITIMISHO ..... 39

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limefanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la mwaka 2023 na Mitaala iliyoboreshwa ya mwaka 2023. Mapitio yaliyofanyika yameonesha kuwa mfumo wa elimu umefanyiwa maboresho ambapo Elimu ya Lazima itaanzia Elimu ya Msingi hadi Elimu ya Sekondari ya chini ambapo mwanafunzi atakayeanza Darasa la Kwanza ataendelea hadi Kidato cha Nne. Mwanafunzi anayehitimu na kufaulu atajiunga na Vyuo vya Kitaalamu vya Kati au Elimu ya Sekondari ya Juu na hatimaye masomo ya Shahada. Maboresho ya Sera ya Elimu yalienda sambamba na maboresho ya Mitaala kwa ngazi ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu. Sera ya Elimu imebainisha kuwa, Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Pili, Darasa la Nne, Darasa la Sita, Kidato cha Pili (Mkondo wa Jumla na Amali), Utahini wa Kidato cha Nne (Mkondo wa Jumla na Amali), Kidato cha Sita na Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi, Elimu ya Awali, Elimu Maalum na Elimu ya Msingi masomo ya Sayansi na Hisabati utafanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani limeandaa Mwongozo wa Utahini na Utunuku kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la mwaka 2023 na Mitaala iliyoboreshwa ya mwaka 2023 kwa lengo la kubainisha taratibu za Uendeshaji na Usimamizi wa Upimaji wa Kitaifa na Utahini wa Mitihani ya Taifa ili kuendana na Sera na Mitaala iliyoboreshwa. Mwongozo huu umezingatia matakwa ya Sera, Mitaala na Waraka wa Elimu Na. 4 Toleo la mwaka 2023. Kwa mujibu wa nyaraka hizo, wanafunzi wa Darasa la Pili, Darasa la Nne, Darasa la Sita na Kidato cha Pili, watafanya Upimaji wa Kitaifa kwa lengo la kubaini kiwango cha umahiri kilichofikiwa ili kufanya urekebifu panapostahili. Kwa Kidato cha Nne na Sita, utahini utafanyika kubaini kiwango cha umahiri cha mtahiniwa kuendelea na ngazi nyingine ya elimu. Kwa upande wa Stashahada ya Ualimu, utahini utafanyika kwa lengo la kubaini kiwango cha umahiri wa walimu tarajali katika taaluma ya ualimu na kuendelea na ngazi nyingine ya elimu.

Mwongozo huu umefafanua namna Upimaji na Utahini utakavyofanyika katika Elimu ya Msingi, Sekondari ya Chini (Mkondo wa Jumla na Amali), Sekondari ya Juu na Stashahada ya Ualimu. Pia, umefafanua

jinsi viwango na madaraja ya ufaulu vitakavyokuwa na jinsi alama endelevu zitakavyopatikana katika Shule ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Mwongozo huu unaanza kutumika kuanzia mwaka 2024.

Baraza la Mitihani linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika maandalizi ya Mwongozo huu. Aidha, Baraza linatoa wito kwa wadau wote wanaosimamia elimu kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa mwongozo huu ili utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la mwaka 2023 na Mitaala iliyoboreshwa ya mwaka 2023 katika eneo la Upimaji na Utahini uweze kufanyika kwa ufanisi.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACSEE | *Advance Certificate of Secondary Education Examination* |
| CA | *Continuous Assessment* |
| CSEE | *Certificate of Secondary Education Examination* |
| DPPEE | *Diploma in Pre-Primary Education Examination* |
| DPEE | *Diploma in Primary Education Examination* |
| DSPEE | *Diploma in Special Education Examination* |
| FE | *Final Examination* |
| FTNA | *Form Two National Assessment* |
| GPA | *Grade Point Average* |
| KKK | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| NACTVET | *National Council for Technical and Vocational Education and Training* |
| NECTA | *National Examinations Council of Tanzania* |
| NTA | *National Technical Award* |
| NVA | *National Vocational Award* |
| PReMS | *Primary Record Manager for Secondary* |
| SFNA | *Standard Four National Assessment* |
| SDPEESM | *Special Diploma in Primary Education Examination in Science and Mathematics* |
| SSNA | *Standard Six National Assessment* |
| STNA | *Standard Two National Assessment* |

## 1.0 UTANGULIZI

Baraza la Mitihani la Tanzania limefanya uchambuzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023, Mitaala iliyoboreshwa na Waraka wa Elimu Namba 4 wa mwaka 2023 kwa lengo la kubainisha maeneo ambayo yanatakiwa kutekelezwa na Baraza la Mitihani pamoja na wadau mbalimbali wa Elimu hasa katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Uchambuzi huo ulibaini kuwa, kwa ujumla maboresho yaliyofanyika ni muhimu sana katika kipindi hiki cha mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na uandaaji wa rasilimali watu inayohitajika katika karne ya 21. Maeneo ambayo yanahitaji Baraza kufanya maboresho ni pamoja na:

(a) Upimaji na Utahini: Sera ya Elimu na Mafunzo inaonesha kuwa muundo wa elimu utakuwa 1+6+4+2/3+3+ ambapo Elimu ya Awali itakuwa mwaka 1, Elimu ya Msingi miaka 6, Elimu ya Sekondari ya Chini (Mkondo wa Jumla na Amali) miaka 4, Elimu ya Sekondari ya Juu miaka 2, Elimu ya Amali (Vyuo vya Kati) miaka 3 na Elimu ya Juu miaka 3+. Kwa kuzingatia muundo huo, Baraza la Mitihani litaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Pili (STNA), Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) na Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita (SSNA) katika ngazi ya Elimu ya Msingi. Kwa upande wa Elimu ya Sekondari ya Chini na Elimu ya Sekondari ya Juu, Baraza litaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) kwa Mkondo wa Jumla na Amali, Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) kwa Mkondo wa Jumla na Amali na Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE). Aidha, Baraza litafanya utahini wa Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali (DPPEE), Stashahada ya Ualimu Elimu Msingi (DPEE), Diploma ya Ualimu Elimu Maalum (DSPEE) na Stashahada Maalum ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa masomo ya Sayansi na Hisabati (SDPEESM).

(b) Fomati za Mitihani: Uchambuzi wa mhutasari ya Mitaala iliyoboreshwa ulionesha kuwa, wanafunzi wa Mkondo wa Jumla na Amali watasoma Historia ya Tanzania na Maadili kama somo la lazima kuanzia Darasa la Kwanza hadi Kidato

cha Sita na Elimu ya Biashara (Business Studies) ngazi ya elimu ya sekondari ya chini. Masomo mengine ni *Additional Mathematics*, Fasihi ya Kiswahili na *Literature in English* ambayo yataanza kufundishwa Kidato cha Tatu. Vilevile, wigo wa masomo ya lugha umepanuliwa kwa kuwepo masomo chaguzi ya Lugha ya Kiarabu, Kichina, na Kifaransa katika ngazi zote za elimu. Somo la Mawasiliano ya Kitaaluma (Academic Communication) na Mawasiliano ya Kitaalamu (Professional Communication) yatakuwa ya lazima kwa ngazi ya Sekondari ya Juu na Stashahada ya Ualimu mtawalia. Aidha, somo la Mbinu za Kufundishia Historia ya Tanzania na Maadili litafundishwa ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi na Elimu Maalumu na halitafundishwa ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali. Msisitizo umewekwa katika upimaji wa umahiri ambapo Baraza la Mitihani limeandaa Mwongozo wa Upimaji na Utahini utakaotumika katika ngazi ya Shule za Msingi, Sekondari na Ualimu.

(c) Mwongozo wa Alama Endelevu (CA): Baraza la Mitihani limefanya maboresho katika mwongozo wa CA kutokana na maboresho ya muundo wa elimumsingi na kuanzishwa kwa masomo mapya katika ngazi mbalimbali za elimu. Maboresho yaliyofanyika yanahusu upimaji utakaochangia katika alama endelevu za mitihani ya Kidato cha Nne Mkondo wa Jumla na Amali, Kidato cha Sita na Stashahada ya Ualimu. Katika Mtihani wa Kidato cha Nne, mchango wa Alama Endelevu (CA) kwa mkondo wa jumla na masomo *bebezi*[1] ya mkondo wa Amali, CA itachangia asilimia 30. Kwa upande wa masomo ya *Fani*[2] na *Computer Applications* mkondo wa Amali, CA itachangia asilimia 60. Vilevile, kwa mitihani ya Kidato cha Sita na Stashahada ya Ualimu itakuwa na mchango wa asilimia 30 kwa masomo yote **isipokuwa** somo la Ualimu kwa Vitendo ambalo litakuwa na mchango wa asilimia 70. Aidha katika Mwongozo wa CA, Baraza la

---

**Bebezi**[1] Ni masomo ambayo yanapaswa kusomwa katika fani ili kufanya ukamilifu wa fani husika. Mfano somo la Kifaransa linalosomwa katika fani ya Utalii na Ukarimu.

**Fani**[2] Ni eneo maalumu la elimu, maarifa au kazi ambayo humtambulisha mtu kutokana na utalaamu wa eneo hilo. Mfano: Fani ya Electrical Engineering humtambulisha mtu kama Electrical Engineer.

Mitihani limebainisha namna ya kuandaa Kazi Mradi na upimaji unaofanyika katika ngazi ya shule pamoja na tathmini ya upimaji wa masomo kwa vitendo ngazi ya shule.

## 2.0 UPIMAJI NA UTAHINI UTAKAOFANYWA NA BARAZA LA MITIHANI

(a) Katika kutekeleza matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023, Mitaala iliyoboreshwa na Waraka wa Elimu Namba 4 wa mwaka 2023 Baraza la Mitihani litafanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Pili, Darasa la Nne, Darasa la Sita, na Kidato cha Pili Mkondo wa Jumla na Amali. Aidha, Baraza litafanya utahini wa Kidato cha Nne Mkondo wa Jumla na Amali, Kidato cha Sita na Stashahada ya Ualimu. Jedwali Na. 1 linabainisha Masomo ya Lazima na Masomo Chaguzi kwa ngazi ya Elimu Msingi na Sekondari ya Juu, masomo mapya na namna Baraza litakavyofanya Upimaji na Utahini.

**Jedwali Na. 1 : Upimaji na Utahini utakaofanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania**

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Darasa la Pili | Umahiri Mkuu; Kusoma; Kuandika; Kuhesabu; Basic English Language Skills; Kuthamini utamaduni, imani, Sanaa na Michezo, Kutunza Afya na Mazingira. | Umahiri Mkuu;<br>(a) Basic English Language Skills.<br>(b) Kuthamini utamaduni, imani, Sanaa na michezo. | (a) Upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK)/Reading, Writing and Arithmetic Assessment (3Rs) utafanyika kwa sampuli katika Shule zitakazobainishwa.<br>(b) NECTA itaandaa Mwongozo na Mfumo utakaowezesha Upimaji wa KKK kwa ngazi ya shule kufanyika katika Shule zote.<br>(c) Upimaji utafanyika kila mwaka.<br>(d) Sababu ya Upimaji ni kubaini Umahiri wa wanafunzi katika Kusoma, Kuandika na Kuhesabu | 2025 |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | na kutoa mrejesho kwa mamlaka husika ili kuboresha zaidi mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji stadi hizo. | |
| 2. | Darasa la Nne | (a) Masomo ya **lazima** ni Kiswahili, English Language, Hisabati, Sayansi, Jiografia na Mazingira, Sanaa na Michezo, Historia ya Tanzania na Maadili na Elimu ya Dini.<br>(b) Masomo **chaguzi** ni French Language,Chinese Language na Arabic Language | (a) Jiografia na Mazingira<br>(b) Sanaa na Michezo<br>(c) Historia ya Tanzania na Maadili<br>(d) French Language<br>(e) Chinese Language<br>(f) Arabic Language | (a) Upimaji utakuwa wa Kitaifa wa Darasa la Nne/Standard Four National Assessment (SFNA).<br>(b) Kwa masomo ya Lugha za kigeni (Kifaransa, Kichina na Kiarabu) mwanafunzi atapimwa somo mojawapo atakalochagua na kusajiliwa.<br>(c) Jumla ya masomo yatakayotahiniwa ni **07** ambapo **06** ni ya lazima na **01** chaguzi. Katika muundo wa upimaji, masomo ya Jiografia na | 2025 |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mazingira na Sanaa na Michezo yataunganishwa na kuitwa somo la **Jiografia na Mazingira Sanaa na Michezo**.<br>(d) Sababu ya Upimaji ni kubaini umahiri wa mwanafunzi katika kumudu masomo yanayofundishwa Darasa la Tatu na la Nne na kuwezesha mamlaka husika kufanya urekebishaji (remediation) kwa mwanafunzi anayebainika kutomudu stadi za KKK au kuwa na umahiri katika masomo husika. | |
| 3. | Darasa la Sita | (a) Masomo ya lazima ni lugha ya Kiswahili, English Language, Hisabati, | (a) Jiografia na Mazingira<br>(b) Sanaa na Michezo | (a) Upimaji utakuwa wa Kitaifa wa Darasa la Sita/Standard Six National Assessment (SSNA). | 2027 |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Sayansi, Jiografia na Mazingira, Sanaa na Michezo, Historia ya Tanzania na Maadili na Elimu ya Dini.<br><br>(b) Masomo chaguzi ni French Language, Chinese Language, Arabic Language | (c) Historia ya Tanzania na Maadili<br>(d) French Language<br>(e) Chinese Language<br>(f) Arabic Language | (b) Kwa masomo ya French Language, Chinese Language, Arabic Language mwanafunzi ataendelea na somo ambalo alipimwa Darasa la Nne (SFNA).<br>(c) Jumla ya masomo yatakayotahiniwa ni **07** ambapo **06** ni ya lazima na **01** chaguzi. Katika muundo wa upimaji masomo ya Jiografia na Mazingira na Sanaa na Michezo yataunganishwa na kuitwa somo la **Jiografia na Mazingira Sanaa na Michezo**.<br>(d) Sababu za Upimaji ni kubaini umahiri, maarifa na stadi alizopata mwanafunzi kuanzia Darasa la Kwanza hadi la | |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Sita na kuwezesha mamlaka husika kufanya uchaguzi (selection) na urekebishaji (remediation) kwa mwanafunzi aliyebainika kutokuwa na umahiri kwa kiwango kilichowekwa. | |
| 4. | Kidato cha Pili | (a) Masomo ya **lazima** kwa **Mkondo wa Jumla** ni **sita (6)** ambayo ni Mathematics, Kiswahili, English Language, Business Studies, Geography na Historia ya Tanzania na Maadili.<br><br>(b) Masomo **chaguzi** kwa **Mkondo wa** | (a) Busines Studies.<br>(b) Historia ya Tanzania na Maadili.<br>(c) Computer Science.<br>(d) Sport studies. | (a) Upimaji utakuwa wa Kitaifa wa Kidato cha Pili/ Form Two National Assessment (FTNA).<br>(b) Wanafunzi wa **Mkondo wa Jumla** watatahiniwa masomo **06** ya lazima, na masomo kati ya **02** hadi **03** kwa kuzingatia **mchepuo** aliochagua. Aidha, atakuwa na fursa ya kuongeza somo **chaguzi** moja kwa watahiniwa wenye masomo ya lazima **09** na | 2025 (Mkondo wa Amali)<br>2026 (Mkondo wa Jumla) |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Jumla** ni: Biology, Arabic Language, Chinese Language, French Language, Computer Science, Textile and Garment Construction, Food and Human Nutrition, Elimu ya Dini ya Kiisalmu, Bible Knowledge, Physics, Chemistry, Sport Studies, Music, Fine Art, Theatre Arts, Book Keeping, Agriculture na History.<br>(c) Michepuo iliyopo katika **Mkondo wa Jumla**: Natural Science, | | **mawili (02)** kwa wenye masomo ya lazima **08**. Hivyo kuwa na jumla ya masomo kati ya **8-10**.<br>(c) Watahiniwa wa **Mkondo wa Amali** watatahiniwa masomo ya lazima **nane (08)** au **tisa (09)** kwa kuzingatia fani aliyochagua.<br>(d) Mwanafunzi ataruhusiwa kuhama mkondo kabla ya kufanya Upimaji wa Kidato cha Pili.<br>(e) Sifa za kuendelea na Kidato cha Tatu kwa kila mkondo (path) zitabainishwa na Baraza la Mitihani katika Kanuni za Mitihani.<br>(f) Watahiniwa wa mfumo usio rasmi wanaohitaji | |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Agriculture, Sport Science, Information and Communication Technology (ICT), Business, Music, Social Science, Arts, Language, Food and Human Nutrition na Textile.<br>(d) Masomo ya **lazima** kwa wote katika **Mkondo wa Amali** ni **sita (06)** Mathematics, English Language, Business Studies, Computer Applications, Life Skills, Historia ya Tanzania na Maadili.<br>(e) Masomo ya **lazima** | | kufanya mtihani wa Kidato cha Nne watafanya upimaji wa Kidato cha Pili wa Mkondo wa Jumla au Mkondo wa Amali kama watahiniwa wa Kujitegemea. | |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kwa fani **Mkondo wa Amali** ni: French Language (Amali za Ukarimu na Utalii), Agriculture na Biology (Amali za Kilimo/ Mifugo), French Language/Chinese/ Arabic Language* (Amali za Sanaa za Maonesho na Amali za Michezo), Engineering Science na Technical Drawing (Amali za TEHAMA, Amali za Kihandisi na Amali za Ushoni).<br><br>*Mwanafunzi ataruhusiwa | | | |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuchagua somo moja kati ya hayo.<br>(f) Fani kuu zilizopo katika **Mkondo wa Amali ni kumi na tano (15)** ambapo mwanafunzi atachagua somo **moja (01)** ambalo ni Fani Mahsusi kutoka katika fani kuu mojawapo. Fani kuu na fani mahususi zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 2**. | | | |
| 5. | Kidato cha Nne | (a) Masomo ya lazima kwa Mkondo wa Jumla ni **sita (6)**: Mathematics, Kiswahili, English Language, | (a) Historia ya Tanzania na Maadili<br>(b) Computer Science<br>(c) Sport Studies | (a) Watahiniwa watafanya Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE).<br>(b) Watahiniwa wa **Mkondo wa Jumla** watatahiniwa jumla ya masomo ya | 2027<br>(Mkondo wa Amali)<br>2028 (Mkondo wa |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Business Studies, Geography na Historia ya Tanzania na Maadili.<br>(b) Masomo chaguzi kwa Mkondo wa Jumla ni: Additional Mathematics, Biology, History, Literature in English Language, Arabic Language, Chinese Language, French Language, Computer Science, Textile and Garment Construction, Food and Human Nutrition, Fasihi ya Kiswahili, Elimu ya Dini ya Kiislamu, | (d) Fasihi ya Kiswahili | lazima **8** hadi **9** (**6** ya lazima na **2-3** ya mchepuo atakaokuwa amechagua). Aidha kwa watahiniwa wa mkondo wa jumla watakuwa na fursa ya **kuchagua masomo ya ziada** yanayoanza kufundishwa Kidato cha Tatu ambayo ni Additional Mathematics, Fasihi ya Kiswahili na Literature in English.<br>(c) Watahiniwa wa **Mkondo wa Amali** watafanya Mtihani wa jumla ya masomo ya lazima **nane (08)** au **tisa (09)** kwa kuzingatia fani aliyochagua.<br>(d) Watahiniwa wa **Mkondo wa Jumla** na **Amali** | Jumla) |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Bible Knowledge, Physics, Chemistry, Sport Studies, Music, Fine Art, Theatre Art, Book Keeping na Agriculture.<br><br>(c) Michepuo iliyopo kwa **Mkondo wa Jumla** ni:<br><br>Natural Science, Agriculture, Sport Science, ICT, Busines, Music, Food and Human Nutrition, Textile, Social Science, Arts na Language.<br><br>(d) Masomo ya **lazima** kwa wote katika Mkondo wa Amali ni **sita (06)** ambayo ni Mathematics, | | wataendelea Kidato cha Tatu na masomo waliyochagua na kupimwa Kidato cha Pili.<br><br>(e) Baraza la Mitihani la Tanzania litatunuku Cheti cha Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) kwa Watahiniwa wa Mkondo wa Jumla na Mkondo wa Amali kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Mitihani Sura ya **107** toleo la 2019 Kifungu cha **5 (3)**.<br><br>(f) Lengo la utahini wa Mtihani wa Kidato cha Nne ni kupima kiwango cha umahiri wa mtahiniwa na kubaini endapo ana mahiri za kuendelea na masomo ya Sekondari ya Juu au Vyuo vya Kati . | |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | English Language, Business Studies, Computer Applications, Life Skills, Historia ya Tanzania na Maadili.<br>(e) Fani kuu zilizopo katika Mkondo wa Amali ni **kumi na tano (15)** ambapo mwanafunzi atachagua somo **moja (01)** ambayo ni Fani Mahsusi kutoka katika fani kuu mojawapo. Fani kuu na fani mahususi zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 2**.<br>(f) Masomo ya lazima | | | |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kwa fani Mkondo wa Amali ni: French Language (Amali za Ukarimu na Utalii), Agriculture na Biology (Amali za Kilimo/ Mifugo), French Language/Chinese/ Arabic Language* (Amali za Sanaa za Maonesho na Amali za Michezo), Engineering Science na Technical Drawing (Amali za TEHAMA, Amali za Kihandisi na Amali za Ushoni).<br><br>*Mwanafunzi ataruhusiwa kuchagua somo | | | |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | moja kati ya hayo. | | | |
| 6. | Kidato cha Sita | (a) Masomo ya **lazima mawili (02)** ambayo ni Historia ya Tanzania na Maadili na Academic Communication.<br>(b) Masomo **chaguzi** ni: History, Geography, Divinity, Elimu ya Dini ya Kiislamu, Kiswahili, English Language, French Language, Chinese Language, Physics, Chemistry, Biology, Food and Human Nutrition, Computer Science, Mathematics, Basic Applied | (a) Historia ya Tanzania na Maadili<br>(b) Academic Communication<br>(c) Sport Studies<br>(d) Fasihi ya Kiswahili<br>(e) Literature in English | (a) Watahiniwa watafanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita (ACSEE).<br>(b) Watahiniwa watatahiniwa jumla ya masomo **05** hadi **07** (**02** ya lazima na **03** tahasusi aliyochagua) na somo **01** la Basic Applied Mathematics kwa tahasusi zenye kigezo cha mtahiniwa kusoma somo hilo. Aidha watahiniwa watapewa fursa ya kuchagua somo **moja (01)** iwapo watakuwa na jumla ya masomo yasiyozidi **sita (06)**.<br>(c) Masomo **chaguzi** ya Kidato cha Tano na Kidato cha Sita | 2027 |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mathemetics (BAM), Agriculture, Sport Studies, Fine Art, Music, Theatre Arts, Textile and Garment Construction, Business Studies, Accountancy, Economics, Fasihi ya Kiswahili, Arabic na Literature in English.<br>(c) Michepuo iliyopo ni Natural Science, Social Science, Language, Business, Sport Studies, Art, na Religious Studies ambayo yanaunda Tahasusi mbalimbali. | | yatatokana na masomo chaguzi aliyofanyia Mtihani wa Kidato cha Nne.<br>(d) Sifa za kutahiniwa Kidato cha Sita zitabainishwa katika Kanuni za Mitihani.<br>(e) Watahiniwa waliosoma somo la Additional Mathematics sekondari ya chini hawatasajiliwa kusoma somo la Basic Applied Mathematics (BAM) katika ngazi ya sekondari ya juu. Aidha wataruhusiwa kusajiliwa katika mojawapo ya somo atakalochagua kutokana na mahitaji yake.<br>(f) Watahiniwa wa Kujitegemea watatakiwa kuwa na angalau *Credit* | |

| Na. | Ngazi ya Elimu | Stadi/Somo Lililobainishwa | Masomo Mapya | Upimaji/Utahini wa Baraza na Sababu | Mwaka wa Kuanza Upimaji/ Utahini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Tatu katika Mtihani wa Kidato cha Nne.<br>(g) Lengo la Mtihani wa Kidato cha Sita ni kupima kiwango cha umahiri wa watahiniwa na kubaini endapo wana umahiri wa kuendelea na masomo ya Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu. | |

**Jedwali Na. 2: Fani Kuu na Mahususi Mkondo wa Amali**

| Na | Fani Kuu | Fani Mahususi |
|---|---|---|
| 1. | Electrical Engineering | (i) Electrical installation |
| | | (ii) Bio-energy installation |
| | | (iii) Wind power plants installation |
| | | (iv) Solar power installation |
| 2. | Mechanical Engineering | (i) Welding and metal fabrication |
| | | (ii) Refrigeration and air conditioning |
| | | (iii) Fitter machinist |
| | | (iv) Fitter mechanics |
| | | (v) Ginnery fitting |
| 3. | Civil Engineering | (i) Masonry and brick-laying |
| | | (ii) Civil drafting |
| | | (iii) Boat building |
| | | (iv) Carpentry and joinery with metal works |
| | | (v) Plumbing and pipe fitting |
| | | (vi) Painting and sign writing |
| | | (vii) Steel fixing |
| | | (viii)Well drilling |
| | | (ix) Wood carving |
| 4. | Automotive Engineering | (i) Motor vehicle mechanics |
| | | (ii) Auto-electric mechanics |
| | | (iii) Auto-body repair |
| | | (iv) Motor-cycle mechanics |
| | | (v) Agro-mechanics |
| 5. | Electronics and Computer | (i) Computer programming |
| | | (ii) Graphics design |
| | | (iii) Electronics repair |
| | | (iv) Computer maintenance |
| | | (v) Mobile phone repair |
| | | (vi) Office machines maintenance |
| | | (vii)Film and TV Production |
| 6. | Transport and Logistics | (i) Transport operations |
| | | (ii) Clearing and forwarding |
| 7. | Clothing and Textile | (i) Handloom weaving |
| | | (ii) Finishing craft |
| | | (iii) Basic knitting |

| Na | Fani Kuu | Fani Mahususi |
|---|---|---|
| | | (iv) Designing, sewing and cloth technology |
| | | (v) Leather goods and footwear |
| 8. | Agriculture and Food Processing | (i) Meat processing and technology |
| | | (ii) Oil seed processing |
| | | (iii) Animal health and production |
| | | (iv) Horticulture production |
| | | (v) Field crop production |
| | | (vi) Wood processing |
| | | (vii) Bee keeping |
| | | (viii) Fishing and fish processing |
| | | (ix) Aquaculture and fish processing |
| | | (x) Seaweed farming |
| 9. | Hospitality and Tourism | (i) Front office operations |
| | | (ii) House-keeping |
| | | (iii) Food production |
| | | (iv) Food beverage services and sales |
| | | (v) Tour guide and travel operations |
| 10. | Commercial and Business Support Services | (i) Business operation assistance |
| | | (ii) Secretarial |
| | | (iii) Insurance |
| | | (iv) Wholesale and retailing |
| | | (v) Geospatial technology |
| 11. | Printing | (i) Packaging printing |
| | | (ii) Screen printing |
| | | (iii) Binding and print finishing |
| 12. | Extraction and Processing of Minerals | (i) Jewellery |
| | | (ii) Salt extraction |
| | | (iii) Gemology (Gemstone cutting, polishing and carving) |
| 13. | Cosmetology | (i) Hair dressing |
| | | (ii) Beauty therapy |
| | | (iii) Fitness and nutrition |
| 14. | Creative Arts | (i) Acting |
| | | (ii) Costume and makeup designs |
| | | (iii) Ngoma performance |
| | | (iv) Music and sound technology |
| | | (v) Music performance |
| | | (vi) Carving |
| | | (vii) Drawing and painting |

| Na | Fani Kuu | Fani Mahususi |
|---|---|---|
| | | (viii) Pottery and ceramic |
| | | (ix) Textile design and small-scale Printing |
| | | (x) Art and design |
| 15. | Sports | (i) Football perfomance |
| | | (ii) Netball perfomance |
| | | (iii) Track events |

(b) Lugha itakayotumika katika Upimaji na Mitihani ngazi ya Elimu ya Msingi (Darasa la Pili, Darasa la Nne na Darasa la Sita) pamoja na Diploma ya Ualimu ni Kiswahili ambayo kwa mujibu wa mtaala ndiyo itatumika katika ufundishaji na ujifunzaji **isipokuwa** kwa somo la English Language, Arabic Language, French Language na Chinese Language. Upimaji wa Kidato cha Pili, Mtihani wa Kidato cha Nne na Kidato cha Sita lugha itakayotumika kutahini ni Kiingereza ambayo itatumika katika ufundishaji na ujifunzaji **isipokuwa** kwa somo la Kiswahili, French Language, Arabic Language, Chinese Language na Elimu ya Dini ya Kiislamu. Aidha, Shule za Msingi, Sekondari na vyuo vya Ualimu vitakavyoidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutumia lugha ya kufundishia ambayo ni tofauti na iliyoelekezwa kwenye Mtaala, Baraza la Mitihani litatahini kwa kutumia lugha aliyotumia mwanafunzi/mtahiniwa katika ufundishaji na ujifunzaji.

(c) Watahiniwa wenye mahitaji maalumu wataandaliwa upimaji na mitihani kwa kuzingatia mitaala iliyoidhinishwa katika ngazi ya elimu husika. Maandalizi ya upimaji na mitihani yatazingatia mahitaji muhimu yanayotakiwa kutokana na aina na kiwango cha ulemavu cha mtahiniwa. Watahiniwa wenye ulemavu wa uoni wataandaliwa mitihani kwa maandishi ya *Braille*, wenye uoni hafifu kwa maandishi yaliyokuzwa, wenye ulemavu wa viungo ambao umeathiri uwezo wao wa kuandika na wengine watakaobainika kuwa na mahitaji maalum wataandaliwa mitihani kulingana na mahitaji yao. Watahiniwa hao

wataongezewa muda wa kufanya Upimaji/Mtihani kwa kuzingatia taratibu za Baraza la Mitihani. Aidha, usimamizi wa uendeshaji wa mitihani ya watahiniwa utahusisha walimu wenye utaalamu wa mahitaji husika.

## 3.0 KUTUNUKU UPIMAJI WA KITAIFA NA MITIHANI YA TAIFA

Baraza la Mitihani limefanya Mapitio ya Madaraja, Mfiko wa Alama, Viwango vya Umahiri na matumizi ya Alama Endelevu (CA) katika upimaji na utahini wa elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu na kufanya maboresho kwa kuzingatia maboresho yaliyofanyika katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la mwaka 2023 na Mitaala iliyoboreshwa ya mwaka 2023.

### 3.1 Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Pili (STNA)

Gredi ya Ufaulu, Mfiko wa Alama na Viwango vya Umahiri katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Pili (STNA) vitatumika kupima stadi **tatu (03)** ambazo ni Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Gredi ya Ufaulu, Mfiko na Viwango vya Umahiri**

| Gredi | Mfiko wa Alama kwa Stadi (50) | Mfiko wa Alama kwa Stadi Tatu (150) | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|---|
| A | 41 – 50 | 121-150 | Bora |
| B | 31 – 40 | 91-120 | Vizuri Sana |
| C | 21 – 30 | 61- 90 | Vizuri |
| D | 11 – 20 | 31- 60 | Inaridhisha |
| E | 0 – 10 | 0 - 30 | Hafifu |

### 3.2 Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) na Darasa la Sita (SSNA)

Gredi ya ufaulu na mfiko wa alama vitatumika kuchakata matokeo ya mwanafunzi kwa kuzingatia idadi ya masomo **sita (06)** kati ya masomo **saba (07)** aliyofaulu vizuri. Hivyo, upangaji wa gredi na mfiko wa alama utazingatia

jumla ya alama **300** kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4: Gredi ya Ufaulu, Mfiko na Viwango vya Umahiri**

| Gredi | Mfiko wa Alama kwa Somo (50) | Mfiko wa Alama kwa Masomo Saba (300) | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|---|
| A | 41-50 | 241 –300 | Bora |
| B | 31-40 | 181 – 240 | Vizuri Sana |
| C | 21-30 | 121 – 180 | Vizuri |
| D | 11-20 | 61 – 120 | Inaridhisha |
| E | 0-10 | 0 – 60 | Hafifu |

## 3.3 Upimaji wa Kitaifa Kidato cha Pili (FTNA) na Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE)

Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) na Mtihani Kidato cha Nne (CSEE) upo katika makundi makuu **mawili (02)** ambayo ni **Mkondo wa Jumla** na **Mkondo wa Amali**. Hivyo, uchakataji na utoaji wa matokeo utazingatia mkondo wa Elimu husika.

### 3.3.1 Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili Mkondo wa Jumla na Mkondo wa Amali

Madaraja ya ufaulu na mfiko wa alama vitatumika kuchakata matokeo ya mwanafunzi aliyefanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa kuzingatia idadi ya masomo **saba (07)** kati ya **nane (08)** hadi **kumi (10)** kwa mkondo wa Jumla na kati ya masomo **nane (08)** au **tisa (09**) kwa mkondo wa Amali ambayo ameyafaulu vizuri. Gredi ya ufaulu, mfiko wa alama, madaraja ya ufaulu na viwango vya umahiri ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 5 – 6.

**Jedwali Na. 5: Gredi ya Ufaulu, Mfiko wa Alama na Viwango vya Umahiri kwa Mkondo wa Jumla na Amali**

| Gredi | Mfiko wa Alama | Pointi | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|---|
| A | 75 – 100 | 1 | Bora |
| B | 65 – 74 | 2 | Vizuri sana |
| C | 45 – 64 | 3 | Vizuri |
| D | 30 – 44 | 4 | Inaridhisha |
| F | 0 – 29 | 5 | Hafifu |

**Jedwali Na. 6: Madaraja ya Ufaulu, Mfiko wa Pointi na Viwango vya Umahiri kwa Mkondo wa Jumla na Amali**

| Daraja | Mfiko wa Pointi | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|
| I | 7 – 17 | Bora |
| II | 18 – 21 | Vizuri sana |
| III | 22 – 25 | Vizuri |
| IV | 26 – 33 | Inaridhisha |

### 3.3.2 Utahini wa Mtihani wa Kidato cha Nne kwa Mkondo wa Jumla na Mkondo wa Amali

Madaraja ya ufaulu na mfiko wa alama vitatumika kuchakata matokeo ya mtahiniwa wa Kidato cha Nne kwa kuzingatia idadi ya masomo **saba (07)** kati ya **nane (08)** au **kumi (10)** kwa Mkondo Jumla na masomo **saba (07)** kati ya **nane (08)** hadi **tisa (09)** kwa Mkondo wa Amali ambayo ameyafaulu vizuri zaidi. Mchanganuo wa Madaraja ya ufaulu na Mfiko wa Alama umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 7 - 9.

**Jedwali Na. 7: Gredi ya Ufaulu, Mfiko wa Alama na Viwango vya Umahiri kwa Mkondo wa Jumla na Mkondo wa Amali (Kwa Masomo yasiyo ya Fani pamoja na Somo la Computer Applications)**

| Gredi | Mfiko wa Alama | Pointi | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|---|
| A | 75 – 100 | 1 | Bora |
| B | 65 – 74 | 2 | Vizuri sana |
| C | 45 – 64 | 3 | Vizuri |
| D | 30 – 44 | 4 | Inaridhisha |
| F | 0 – 29 | 5 | Hafifu |

**Jedwali Na. 8: Gredi ya Ufaulu, Mfiko wa Alama na Viwango vya Umahiri kwa Masomo ya Fani na Somo la Computer Applications**

| Gredi | Mfiko wa alama | Pointi | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|---|
| A | 90 - 100 | 1 | Bora |
| B | 80 - 89 | 2 | Vizuri sana |
| C | 70 -79 | 3 | Vizuri |
| D | 60 - 69 | 4 | Inaridhisha |
| F | 0 - 59 | 5 | Hafifu |

**Jedwali Na. 9: Madaraja ya Ufaulu, Mfiko wa Pointi na Viwango vya Umahiri kwa Mkondo wa Jumla na Amali**

| Daraja | Mfiko wa Pointi | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|
| I | 7 – 17 | Bora |
| II | 18 – 21 | Vizuri sana |
| III | 22 – 25 | Vizuri |
| IV | 26 – 33 | Inaridhisha |

### 3.3.3 Matumizi ya Alama Endelevu Mkondo wa Jumla na Mkondo wa Amali

(a) Katika mtihani wa Kidato cha Nne, ukokotoaji wa Alama ya Mwisho utazingatia Alama Endelevu (CA) na alama aliyopata mtahiniwa katika Mtihani wa Taifa. Uwiano wa **30:70** utatumika kukokotoa Alama ya Mwisho (Final Score); ambapo asilimia **30** ni Alama Endelevu (CA) kutoka shuleni na asilimia **70** ni Alama za Mtihani wa Taifa (FE). Aidha, kwa masomo ya Fani na Somo la Computer Applications kwa Mkondo wa Amali, CA itachangia asilimia **60** na Mtihani wa mwisho utachangia asilimia **40**. Alama ya Mwisho itapatikana kwa kujumlisha alama iliyokokotolewa kutoka katika CA na Mtihani wa Taifa (FE). Alama endelevu za mtahiniwa zitapatikana kuanzia ngazi ya Elimu ya Msingi ambapo Upimaji wa Darasa la Sita (SSNA) utachangia asilimia **05** na hivyo mahiri za masomo ngazi ya elimu ya msingi kuwa na mchango katika ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne. Kazi Mradi, Mitihani ya Mihula Kidato cha Tatu na Mtihani wa Utayari (Mock) itachangia zaidi ya asilimia **63** ya Alama endelevu. Aidha Kazi mradi imeongezewa asilimia **02** na hivyo kuwa na asilimia **07** ikilinganishwa na asilimia **05** iliyotumika katika mtaala wa zamani (kabla ya maboresho ya 2023).

(b) Idadi ya masomo **19** kati ya **28** ambayo ni Biology, Physics, Chemistry, Agriculture, Food and Human Nutrition, History, Bussiness Studies, Book-Keeping, Textile, Music, Fine Arts, Theatre Arts, Engineering Science, Technical Drawing, Life Skills, Computer Applications na Computer Science katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) na masomo ya Fani **15** (Rejea Jedwali Na. 2) za Amali yatakosa CA za Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita (SSNA) kwa kuwa masomo hayo yanaanza kufundishwa Kidato cha Kwanza. Aidha, masomo ya Fasihi ya Kiswahili, Literature in English na Additional Mathematics yanaanza kufundishwa Kidato cha Tatu. Hivyo CA za masomo hayo zitaanza kuchukuliwa kuanzia mwaka ambao somo hilo litaanza kufundishwa.

Uzito wa Alama katika CA, ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 10 hadi 13.

**Jedwali Na. 10: Mchango wa Alama Endelevu (CA) Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) kwa masomo yanayofundishwa kuanzia ngazi ya Elimu ya Msingi**

| Aina ya Upimaji | Mchango wa Upimaji | Mtihani wa Taifa | Maoni |
|---|---|---|---|
| Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita (SSNA) | 5.0% | **70%** | *Pass/Fail* |
| Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) | 6.0% | | |
| Mtihani wa Mwisho wa Mwaka (Kidato cha Tatu) | 5.0% | | |
| Upimaji wa Utimilifu wa Mkoa (Mock) | 7.0% | | |
| Kazi Mradi (somo chaguzi) | 7.0% | | |
| | **30%** | | |

**Jedwali Na.11: Mchango wa Alama Endelevu (CA) kwa Masomo yanayoanza kufundishwa Kidato cha Kwanza Mkondo wa Jumla na Amali**

| Aina ya Upimaji | Mchango wa Upimaji | Mtihani wa Taifa | Maoni |
|---|---|---|---|
| Kidato cha Pili (FTNA) | 6.0% | **70%** | *Pass/Fail* |
| Mtihani wa Mhula wa Kwanza (Kidato cha Tatu) | 5.0% | | |
| Mtihani wa Mwisho wa Mwaka (Kidato cha Tatu) | 5.0% | | |
| Upimaji wa Utimilifu wa Mkoa (Mock) | 7.0% | | |
| Kazi Mradi (somo chaguzi) | 7.0% | | |
| **Jumla** | **30%** | | |

**Jedwali Na. 12: Mchango wa Alama Endelevu (CA) kwa Masomo yanayoanza kufundishwa Kidato cha Tatu Mkondo wa Jumla na Amali**

| Aina ya Upimaji | Mchango wa Upimaji | Mtihani wa Taifa | Maoni |
|---|---|---|---|
| Mtihani wa Mhula wa Kwanza Kidato cha Tatu | 5.0% | **70%** | *Pass/Fail* |
| Mtihani wa Mwisho wa Mwaka (Kidato cha Tatu) | 5.0% | | |
| Mtihani wa Mhula wa Kwanza (Kidato cha Nne) | 6.0% | | |
| Upimaji wa Utimilifu wa Mkoa (Mock) | 7.0% | | |
| Kazi Mradi (somo chaguzi) | 7.0% | | |
| **Jumla** | **30%** | | |

**Jedwali Na. 13: Mchango wa CA Masomo ya Fani na Computer Applications Mkondo wa Amali**

| Aina ya Upimaji | Mchango wa Upimaji | Mtihani wa Kitaifa | Maoni |
|---|---|---|---|
| Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) | 6.0% | **40%** | *Pass/Fail* |
| Upimaji wa Muhula wa Kwanza Kidato cha Tatu | 5.0% | | |
| Upimaji wa Muhula wa Pili Kidato cha Tatu | 5.0% | | |
| Upimaji wa Utimilifu wa Mkoa (Mock) | 7.0% | | |
| Kazimradi (Project) | 7.0% | | |
| Mazoezi kwa Vitendo (Practicals) Kidato cha Pili | 10.0% | | |
| Mazoezi kwa Vitendo (Practicals) Kidato cha Tatu | 10.0% | | |
| Mazoezi kwa Vitendo (Practicals) Kidato cha Nne | 10.0% | | |
| **Jumla** | **60%** | | |

### 3.4 Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita (ACSEE)

Madaraja ya ufaulu na mfiko wa alama vitatumika kuchakata matokeo ya mtahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) kwa kuzingatia idadi ya masomo **matatu (03)** ya tahasusi na ukokotoaji wa Alama ya Mwisho utazingatia Alama Endelevu (CA) na alama aliyopata mtahiniwa katika mtihani wa Taifa kwa uwiano wa **30:70**; ambapo asilimia **30** ni Alama Endelevu (CA) kutoka shuleni na asilimia **70** ni Alama za Mtihani wa Taifa (FE). Mchanganuo wa Madaraja ya ufaulu, mfiko wa alama na viwango vya umahiri na alama za CA ni kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 14 hadi 16.

**Jedwali la 14: Gredi za Ufaulu, Mfiko wa Alama na Viwango vya Umahiri**

| Gredi | Mfiko wa Alama | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|
| A | 80-100 | Bora |
| B | 70-79 | Vizuri Sana |
| C | 60-69 | Vizuri |
| D | 50-59 | Wastani |
| E | 40-49 | Inaridhisha |
| S | 35-39 | Hairidhishi |
| F | 0-34 | Feli |

**Jedwali la 15: Madaraja ya Ufaulu, Mfiko wa Pointi na Viwango vya Umahiri**

| Daraja | Mfiko wa Pointi | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|
| I | 3-9 | Bora |
| II | 10-12 | Vizuri sana |
| III | 13-17 | Vizuri |
| IV | 18-19 | Inaridhisha |

**Jedwali Na. 16: Alama Endelevu kwa Mitihani ya Kidato cha Sita**

| Na. | Aina ya Upimaji | Mchango wa Upimaji | Mtihani wa Mwisho |
|---|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Mhula wa kwanza wa Kidato cha Tano | 5.0% | **70%** |
| 2 | Mtihani wa Mwisho wa mwaka wa Kidato cha Tano | 5.0% | |
| 3 | Mtihani wa Mhula wa Kwanza wa Kidato cha Sita | 6.0% | |
| 4 | Kazi Mradi | 7.0% | |
| 5 | Upimaji wa Utimilifu wa Mkoa (Mock) | 7.0% | |
| **Jumla** | | **30.0%** | |

## 3.5 Mitihani ya Stashahada za Ualimu

### 3.5.1 Aina za Stashahada za Masomo yatakayotahiniwa

Mitihani ya Ualimu itakuwa na Stashahada **nne (4)** ambazo ni Elimu ya Msingi, Elimu Maalumu, Elimu ya Awali na Stashahada Maalum ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa masomo ya Sayansi na Hisabati.

Watahiniwa katika kila Stashahada watatahiniwa masomo **manne (4)** ya msingi ambayo ni; Ualimu (Upimaji na Tathmini, Saikolojia na Sosholojia ya Elimu, Mitaala na Ufundishaji na Falsafa na Maadili ya Ualimu), Elimu Jumuishi, Mawasiliano ya Kitaalamu kwa Walimu, na Ualimu kwa Vitendo. Utahini kwa Mtihani wa Ualimu utafanyika kama ifuatavyo;

(a) **Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi**

Utahini utafanywa katika masomo **sita (6)**; **manne (4)** ya msingi na **mawili (2)** ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ambayo mwalimu tarajali atachagua katika Tahasusi yake aliyosoma Kidato cha VI. Kwa walimu tarajali waliosoma tahasusi za Sanaa, watakuwa na masomo chaguzi kama ifuatavyo:

(i) Masomo mawili ya Mbinu za Ufundishaji kutoka katika masomo ya Tahasusi; **au**

(ii) Somo moja la Mbinu za ufundishaji kutoka katika Masomo ya Tahasusi na Mbinu za Ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania.

(b) **Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu**

Utahini utafanywa katika masomo **saba (7)**; **manne (4)** ya msingi na **matatu (3)** chaguzi ambapo mwalimu tarajali atachagua somo **moja (1)** la mbinu kutoka tahasusi aliyosoma

Kidato cha VI na masomo **mawili (2)** kutoka katika fani za Elimu zilizobainishwa kati ya Uziwi, Uziwikutoona, Uoni, Usonji na Ulemavu wa Akili.

(c) **Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali**

Utahini utafanywa katika masomo **matano (5)**; **manne (4)** ya msingi na **moja (1)** la mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Awali, Darasa la I na II.

(d) **Stashahada Maalum ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa masomo ya Sayansi na Hisabati**

Utahini utafanywa katika masomo **sita (6)**; **manne (4)** ya msingi na **mawili (2)** ya mbinu ambayo ni Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Hisabati na Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Sayansi.

### 3.5.2 Madaraja ya Ufaulu Mtihani wa Ualimu

Madaraja ya Ufaulu na Mfiko wa Alama katika Mtihani wa Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi/Diploma in Primary Education Examination (DPEE); Stashahada ya Ualimu wa Elimu Maalumu/Diploma in Special Education Examination (DSPEE) na Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Awali/Diploma in Pre-Primary Education Examination (DPPEE) na Stashahada Maalumu ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa masomo ya Sayansi na Hisabati/Special Diploma in Primary Education in Science and Mathematics (SDPEESM) vitazingatia idadi ya masomo ya lazima kwa kila mtihani. Mchanganuo wa Madaraja ya Ufaulu, Mfiko wa Alama na Viwango vya umahiri ni kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 17.

**Jedwali Na. 17: Gredi, Mfiko wa Alama na Viwango vya Umahiri**

| Gredi | Pointi | Mfiko wa Alama | Viwango vya Umahiri |
|---|---|---|---|
| A | 5 | 80-100 | Bora |
| B | 4 | 70-79 | Vizuri Sana |
| C | 3 | 55-69 | Vizuri |
| D | 2 | 40-54 | Inaridhisha |
| F | 1 | 0-39 | Feli |

Madaraja ya ufaulu Ngazi ya Stashahada ya Ualimu yapo katika mfumo wa *Grade Point Average* (GPA) ambayo ni *Distinction*, *Credit* na *Pass*. Daraja la *Distinction* ni la ufaulu wa juu na Daraja la *Pass* ni la ufaulu wa chini. Mchanganuo wa Madaraja kwa kutumia *Grade Point Average* (GPA) ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 18. Aidha, uzito wa pointi katika gredi ni; A = 5, B = 4, C = 3, D=2, F = 1.

**Jedwali Na. 18: Madaraja ya Ufaulu**

| **Daraja** | **GPA** | **Viwango vya Umahiri** |
|---|---|---|
| Distinction | 4.4-5.0 | Bora |
| Credit | 3.5-4.3 | Vizuri Sana |
| Pass | 2.0-3.4 | Vizuri |

Ukokotoaji wa *Grade Point Average* (GPA) kwa mtahiniwa wa Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi na Stashahada Maalumu ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa masomo ya Sayansi na Hisabati utafanyika kwa masomo **sita (06)** na Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu utafanyika kwa masomo **saba (07)**. Aidha, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali utafanyika kwa masomo **matano** (**05**) kwa kuzingatia wastani wa Pointi za masomo husika.

GPA itapatikana kwa kukokotoa pointi za masomo aliyofanya mtahiniwa kwa Kanuni ifuatayo:

$$GPA = \frac{\sum p}{n}$$

$\sum$ **=** *summation notation*
***P*** = *pointi za masomo aliyofanya mtahiniwa.*
***n*** = *idadi ya masomo aliyofanya mtahiniwa.*

### 3.5.3 Mchango wa Alama Endelevu katika Mitihani ya Ualimu

Alama Endelevu (CA) ina mchango wa asilimia **30** katika masomo yote ya Ualimu **isipokuwa** somo la Ualimu kwa Vitendo ambalo lina mchango wa asilimia **70**. Mchanganuo wa Alama Endelevu kwa masomo ya Ualimu na Ualimu kwa Vitendo umebainishwa katika Jedwali Na. **19** na **20** mtawalia.

**Jedwali Na. 19: Alama Endelevu kwa Masomo ya Ualimu**

| **Na.** | **Aina ya Upimaji** | **Mchango wa Upimaji** | **Mtihani wa Mwisho** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mtihani wa Mhula wa Kwanza wa Mwaka wa Kwanza | 6.0% | **70%** |
| 2. | Mtihani wa mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0% | |
| 3. | Mtihani wa Mhula wa Kwanza wa Mwaka wa Pili | 6.0% | |
| 4. | Mkoba wa Kazi | 5.0% | |
| 5. | Kazi Mradi | 7.0% | |
| **Jumla** | | **30.0%** | |

**Jedwali Na. 20 : Alama Endelevu kwa Somo la Ualimu kwa Vitendo**

| **Na.** | **Aina ya Upimaji** | **Mchango wa Upimaji** | **Mtihani wa Mwisho** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mtihani wa Mhula wa Mwisho wa Mwaka | 10.0% | |
| 2. | Kazi Mradi ya Ufaraguzi | 15.0% | |

| Na. | Aina ya Upimaji | Mchango wa Upimaji | Mtihani wa Mwisho |
|---|---|---|---|
| 3. | Ufundishaji Igizi | 20.0% | **30%** |
| 4. | Ufundishaji katika Shule ya Jirani | 25.0% | |
| **Jumla** | | **70.0%** | |

## 4.0 UTARATIBU WA KUTUNUKU VYETI

Watahiniwa watatunukiwa Cheti cha Kitaaluma cha Kidato cha Nne (CSEE) Mkondo wa Jumla na Mkondo wa Amali, Kidato cha Sita (ACSEE) na Stashahada ya Ualimu kitakachoakisi masomo waliyotahiniwa.

## 5.0 UTHIBITI NA USIMAMIZI WA ALAMA ENDELEVU

Kutokana na umuhimu wa mchango wa alama endelevu katika mtihani wa mwisho, vigezo vya uthibiti na usimamizi wa alama endelevu vimebainishwa katika Mwongozo wa Alama Endelevu ulioandaliwa. Lengo ni kuhakikisha alama zinazopatikana ni thabiti na zenye kuaminika. Katika mwongozo huo Walimu wa Shule/Vyuo wamepewa maelekezo ya mambo ya msingi ya kuzingatia kuhakikisha Upimaji wa Ndani (School Based Assessment) wa wanafunzi/wanachuo unaimarishwa. Aidha kwa masomo ya Sayansi Vitendo (Practicals for Science Subjects) walimu wanapaswa kuwapima wanafunzi ipasavyo kwa kuzingatia maelekezo katika Mwongozo wa Alama Endelevu na kuhakikisha kuwa, alama za masomo ya vitendo zinajumuishwa katika somo husika.

### 5.1 Usimamizi wa Upimaji na Mitihani Ngazi ya Shule

Wakati wa Uendeshaji wa Upimaji katika Shule na Vyuo vya Ualimu, yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa kwa mujibu wa mwongozo wa Alama Endelevu.

(a) Wanafunzi/Wanachuo wote wa ngazi husika lazima wafanye upimaji wa aina moja katika mazingira yanayofanana.

(b) Muda wa Upimaji uwe wa kutosha kuwawezesha wanafunzi kuonesha ujuzi wao walioupata katika ujifunzaji.

(c) Shule/Vyuo vitoe kalenda inayoonesha tarehe za Upimaji au Mtihani wa mhula au wa mwisho wa mwaka.

### 5.2 Ujazaji na Uwasilishaji wa CA za Wanafunzi/ Wanachuo

Ujazaji na uwasilishaji wa CA za wanafunzi utafanywa katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) **Mwalimu/Mkufunzi wa Somo**

Mwalimu/Mkufunzi wa somo anapaswa:

(i) Kuingiza alama endelevu za mwanafunzi/mwanachuo katika fomu iliyopakuliwa kutoka mfumo wa PReMS wa NECTA na Kadi ya matokeo ya jumla ya mwanafunzi kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.

(ii) Kutunza kumbukumbu za mitihani ya muhula na ya mwisho wa mwaka katika faili la mwanafunzi.

(iii) Kuwasilisha nakala ya alama za mitihani ya muhula na ya mwisho wa mwaka katika ofisi ya taaluma.

(b) **Mkuu wa Shule/Mkuu wa Chuo**

Mkuu wa Shule au Mkuu wa Chuo ana wajibu wa:

(i) Kupandisha kwenye mfumo wa PReMS fomu ya CA iliyojazwa bila kufanya mabadiliko yoyote.

(ii) Kuzalisha na kuchapa fomu za CA za mwanafunzi kutoka katika mfumo wa PReMS. Mkuu wa Shule/Chuo na mwanafunzi wanapaswa kuhakiki usahihi wa fomu ya CA iliyojazwa na kuchapwa kabla ya

kusaini na kuwasilisha nakala ngumu na laini Baraza la Mitihani.

### 5.3 Upimaji na Upatikanaji wa Alama za Kazi Mradi

Baraza la Mitihani litatumia Alama Endelevu za Kazi Mradi ili kuwapima wanafunzi juu ya wanachojifunza kupitia Kazi Mradi, hivyo kubaini mafanikio yao katika stadi mbalimbali. Kazi Mradi lazima iendane na muhtasari wa somo husika ikijumuisha masuala mtambuka ya Sayansi, Teknolojia na Kiuchumi. Mwongozo wa upatikanaji wa alama za Kazi Mradi ni kama ifuatavyo:

(a) Fomati ya taarifa ya Kazi Mradi (10%)

- (i) Kichwa cha Habari
- (ii) Shukrani
- (iii) Jedwali la Yaliyomo
- (iv) Yaliyomo kwenye Sura (Utangulizi, Lengo, Umuhimu wa Kazi Mradi, Njia zilizotumika, Uwasilishaji wa Matokeo, Mjadala, Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo).
- (v) Kumbukumbu na Viambatisho (Pale vinapohitajika).

(b) Ukusanyaji na uchambuzi wa data (40%)

- (i) Usahihi katika kuchunguza
- (ii) Matokeo sahihi ya Utafiti
- (iii) Upangaji wa dhana mbalimbali katika mtiririko wenye mantiki
- (iv) Usahihi na uchambuzi wa data.

(c) Ubora na usahihi wa Kazi Mradi (50%)

- (i) Uchambuzi wa kina wa data na tafsiri yake.
- (ii) Uwiano katika matokeo ya Kazi Mradi, Kujumuisha vielelezo saidizi kama vile ramani, michoro na majedwali.
- (iii) Ubora wa kazi (Nadhifu, usahihi wa kisarufi, matumizi sahihi ya alama za kisarufi n.k)
- (iv) Uasili na upya wa maarifa
- (v) Hitimisho.

Mwongozo wa Alama Endelevu umebainisha vigezo vya kuzingatiwa na walimu/wakufunzi katika kutoa alama kwa kila hatua.

### 5.4 Ufuatiliaji na Tathmini ya Alama Endelevu

Baraza la Mitihani la Tanzania litafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo wa Alama Endelevu Shuleni na Vyuoni ili kutathmini uhalali na matumizi ya kuaminika ya zana zilizotumika kupima wanafunzi/wanachuo. Pia Baraza la Mitihani litachukua sampuli za Kazi Mradi ili kuona kama zimetahiniwa kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa.

## 6.0 HITIMISHO

Mwongozo wa Utahini na Utunuku kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la 2023 na Mitaala iliyoboreshwa ya mwaka 2023 umeandaliwa kwa lengo la kuonesha dira kuhusu namna upimaji na tathmini ngazi ya elimu ya msingi, Sekondari Ngazi ya Chini (Mkondo wa Jumla na Amali), Sekondari ya Juu na Vyuo vya Ualimu itakavyofanyika. Katika utekelezaji wa mwongozo huu, wadau wote wa elimu wanaaswa kuzingatia taratibu za utahini zilizobainishwa ili kufikia malengo yaliyobainishwa katika sera na Mitaala iliyoboreshwa. Baraza la Mitihani la Tanzania litafanya ufuatiliaji wa kina ili kuhakikisha kuwa malengo yote yaliyobainishwa yanatekelezwa ipasavyo.